

Buriani Biwott

Tumefikwa na tanzia, nyoyo mejaa huzuni,
Wenzetu wanajifia, tunalia machozini,
Tumebakil kulia, yatokea siamini!
Biwott buriani, taonana kwa Manani.

Kifo katili sikia, wizi bila samahani,
Ja muwizi waingia, twaa hadi kaburini,
Wapenduwa wavamia, na husiti safarini,
Biwott buriani, taonana kwa Manani.

Biwott twasikitikia, twakosa matumaini,
Twaishi na kuishia, yajapo yapokeeni,
Leo u tele afia, haki kesho taabani,
Biwott buriani, taonana kwa Manani.

Wengi ulisaidia, shule nyangi lidhamini,
Zahanati za afia, ukajenga mashinani,
Wazazi jifungulia, salama na salimini,
Biwott buriani, taonana kwa Manani.

JOSPHAT CHERUIYOT
Chuo Kikuu cha SEKU, Kitu